# SOKO LA BIDHAA TANZANIA
# UTARATIBU WA MAUZO YA KOROSHO GHAFI MSIMU 2025/26.

## 1) Utangulizi

Katika msimu wa mauzo 2025/26 Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa kushirikiana na halmashauri za mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri husika zitasimamia uendeshaji wa minada ya Korosho Ghafi (KOROSHO GHAFI) katika ghala zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Katika msimu huu Korosho Ghafi itauzwa katika njia ya Kidigitali kupitia Mfumo wa soko la bidhaa Tanzania (OTS) katika Mikoa yote ya Tanzania Bara inayolima Korosho Ghafi. Mauzo hayo yanalenga kuleta bei zenye ushindani wa haki, uwazi na kupunguza gharama za ununuzi wa mazao. Wanunuzi wote wa ndani na wa nje,wadogo na wakubwa wanakaribishwa kushiriki kwenye minada itakayoanza karibuni.

## 1) Majukumu ya Mnunuzi

i. Kuzingatia Sheria Na. 18 ya 2009 ya Bodi ya Korosho Tanzania, Sheria Na. 6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013, Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura ya 339 ya Mwaka 2016, pamoja na Sheria ya Soko la Bidhaa ya Mwaka 2015, katika msimu husika.

ii. Kukamilisha hatua za usajili na kupata Leseni ya ununuzi wa Korosho Ghafi kwa msimu 2025/26 kutoka CBT.

iii. Kujaza fomu ya tamko la mnunuzi (BDF) kwa utaratibu uliowekwa na TMX na kuiwasilisha TMX kupitia barua pepe **tmxplc@gmail.com**.

iv. Kupitia Katalogi ya Mauzo '*Sales Catalogue*' na kuweka kiwango cha bei anayotaka kununua Korosho Ghafi kwa njia ya kielektroniki wakati wa mnada. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki wasiliana na TMX kupitia simu namba **+255 713 298 314** au **+255 658 420 742.**

v. Wabanguaji wa ndani ya nchi watanunua kiasi chochcote kwenye kadri itakavyo elekezwa na CBT.

**NB:** Mnunuzi hata ruhusiwa kushiriki minada ya Korosho Ghafi kwenye mfumo wa mauzo wa TMX endapo atakuwa hajakamilisha hatua ya usajili kutoka CBT kwa msimu 2025/26

## 3.0 Hatua za Ununuzi

i. Wanunuzi kujaza fomu ya tamko la mnunuzi (BDF);

ii. Mnunuzi kusajiliwa kwenye mfumo wa mauzo baada ya kuthibitishwa na CBT;

iii. Mnunuzi hataruhusiwa kununua kiasi cha Korosho Ghafi zaidi ya kiwango cha kinga ya dhamana iliyowekwa;

iv. TMX kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika kuandaa Hati ya Mauzo (sales catalogue);

v. Hati ya Mauzo itatumwa kwa wadau ndani ya **masaa 12** kabla ya mnada baada ya uhakiki kufanyika na timu itakayoundwa, Nyongeza ya Hati ya Mauzo itatolewa **saa 1** kabla ya mnada kuanza;

vi. Taarifa za sales catalogue zinaingizwa kwenye mfumo wa mauzo. Mauzo yatafanyika kwa kuzingatia Lot kama zilivyopangwa kwenye ghala la mnada;

vii. Mfumo Wa Mauzo uitafunguliwa kwa ajili ya wanunuzi wenye kupenda kufanya PreBid (Kuweka bei zao kabla ya mnada kuanza) bei hii itaonekana kwa mnunuzi tu mpaka pale muda wa mnada mubashara kuanza;

viii. Minada kufanyika mubashara kupitia mfumo wa mauzo, bei ya juu iliyopatikana wakati wa Pre-bid ndio bei itakayoanzia kwenye lot husika kwa wanunuzi kuanza kushindana;

ix. Wanunuzi kushindana kununua kwa Lot, Lot moja ikitumia muda wa **sekunde 60** (*dakika 1*) na endapo mnunuzi ameweka bei basi itarudi **sekunde 40** mpaka ziishe bila mnunuzi mwingine kuweka bei;

x. Lot moja ikiwa ni kiasi chote cha mazao uliowasilishwa na AMCOS husika au mgawanyo kufuatia uwingi wa zao kwenye ghala la mnada. Mnunuzi anawajibika kununua Lot yote kama ilvyo;

xi. Chama Kikuu cha Ushirika kwa niaba ya wauzaji kuridhia au kukataa bei zilizopatikana kwenye mfumo wa mauzo ndani ya nusu saa baada ya mnada kuisha;

xii. TMX kutoa taarifa ya minada kwa wadau ikionyesha kiasi na bei ya mazao yaliyonunuliwa;

xiii. Chama Kikuu kitaandaa na kutoa ankara ya mauzo (sales invoice) kwa mnunuzi ndani ya **saa 24** baada ya mnada kumalizika;

xiv. Wanunuzi kufanya malipo ya fedha zao ndani ya **saa 120** (*siku 5*) za kazi tangu tarehe ya mnada husika kwenye akaunti za malipo kama zilivyo ainishwa kwenye hati ya madai;

xv. Endapo mnunuzi atashindwa kukamilisha malipo kwa muda, Lot itauzwa tena mnada unaofata kama ilivyo elezwa kwenye **mwongozo na 1 wa usimamizi wa masoko na mauzo ya korosho ghafi kupitia stakabadhi ghalani msimu wa mauzo 2025/2026;**

xvi. Mnunuzi atahitajika kufanya malipo kama **gharama ya uendeshaji** ambayo isiyokuwa bei ya ununuzi kama inavyoonyeshwa kwenye **hati ya madai na "*Cashewnut Board of Tanzania summary of the rules and sales conditions for 2025/26 crop season*";**

xvii. Mnunuzi atapewa agizo la toleo (Release Warranty) na Chama Kikuu baada ya kuamilisha malipo yote kwa mujibu wa ankara ya mauzo;

xviii. Mnunuzi ata takiwa kutoa Korosho Ghafi kwenye ghala ndani ya **siku 14** (zikijumuisha jumamosi na jumapili) tangu tarehe ya kumaliza muda wa malipo. Siku hizi zitaanza kuhesabiwa baada ya **siku 5** za malipo;

xix. Mnunuzi ana haki ya kuhakiki mzigo wake kabla ya kupakia kwenye gari. Mnunuzi atawajibika kujaza hati ya kukiri kuwa amepokea korosho ghafi katika hali ya ubora na uzito kama ilivyo ainishwa. Endapo mnunuzi atapata changamoto za ubora na upungufu wa uzito awasilishe CBT kwa hatua zaidi;

xx. Korosho ghafi zitakazo uzwa katika mikoa ya **Mtwara, Lindi na Ruvuma** zitasafirishwa kupitia **Bandari ya Mtwara**, Aidha, kwa korosho za **maeneo mengine** usafiririshwaji unaweza kufanyika kupitia **Bandari za Mtwara, Dar es Salaam na Tanga**;



.............................................................................................

**IMETOLEWA NA AFISA MTENDAJI MKUU**
**SOKO LA BIDHAA TANZANIA**

**TAREHE 20/10/2025**

Kwa maelezo ya jumla wasiliana na TMX kupitia: info@tmx.co.tz au namba ya simu ifuatayo;

+255 22 2923700.

**Tanzania Mercantile Exchange PLC, P.O. Box 31632, Dar es Salaam, TANZANIA,**
**Email: info@tmx.co.tz, website: www.tmx.co.tz**